CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA
S.L.P 35928,**DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: +255 22 2401581, **Nukushi:** +255 22 2401582
Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz**Tovuti**: www.thtu.or.tz

HII BANDIKA BANDUA ISIPOANGALIWA HARAKA ITADHOOFISHA USTAWI WA WAFANYAKAZI

1. Utangulizi

Miezi hii mitatu; yaani wa saba, wa nane na wa tisa mwaka huu wa 2022 imekuwa michungu sana kwa wafanyakazi na Watanzania kwa ujumla. Uchungu huu umetokana na matukio/masuala yaliyojitokeza kwa kipindi hiki ambayo hayakidhi matarajio wala kiu ya wafanyakazi. Mambo hayo ni; nyongeza ya mishahara, sintofahamu ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na tukio la sasa la Tozo. Matukio haya matatu yamejitokeza kwa kufuatana ndani ya kipindi hiki kifupi (Bandika bandua) kiasi kwamba imewaacha wafanyakazi katika lindi kubwa la mkanganyiko. Kwa sababu mambo haya yanagusa maslahi ya wafanyakazi moja kwa moja, yasipoangaliwa yatahafifisha morali ya utendaji kazi na hivyo kuzorotesha utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Taifa letu.

Ni ukweli usiopingika kwamba watu na wadau mbalimbali wamejitokeza kusemea, kushauri, kukosoa na pia kutoa njia mbadala ya namna ya kurekebisha au kurudisha hali kuwa ya kawaida. Katika kuendelea kuweka uzito na msisitizo, sisi THTU tunapenda kuongeza yafuatayo katika matukio hayo matatu kama ifuatavyo;

2. Ukweli kuhusu Nyongeza ya Mishahara Julai 2022

Serikali iliongeza mishahara ya kima cha chini kwa asilimia 23.3 mwezi Julai. Pamoja na hili kufanyika, upo ukweli ambao ni lazima usemwe ili kutupa nafasi ya kurekebisha wakati ujao kama ifuatavyo;

a. Tofauti na uzoefu wa miaka ya nyuma, nyongeza ya mshahara kwa mwaka huu ina mkanganyiko mkubwa kwani haijafuata mtiririko na uhalisia uliozoeleka kwamba kila mtu/kundi linapata nyongeza ya asilimia kulingana na kiwango cha mshahara husika

b. Baadhi ya wafanyakazi hawajapata nyongeza kabisa hasa wale wenye mishahara binafsi wakati nyongeza ya mishahara huwa inajumuisha watu wote tofauti na nyongeza ya mwaka ambayo ingewatenga wa mshahara binafsi

c. Wafanyakazi wote katika mashirika ya umma kama taasisi za elimu ya Juu walipewa nyongeza sawa bila kujali tofauti zao hivyo kupoteza uhalisia wa nyongeza ya kima cha chini
d. Ni ukweli usiopingika kwamba wafanyakazi walio wengi HAWAJARIDHIKA KABISA na nyongeza iliyotolewa. Kilichopo ni utulivu wa maumivu na sonona na kwamba kumbukumbu hii itabakia.

Hali hii inaweza kurekebishwa kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza mishahara kwenye bajeti ya mwaka ujao ambayo maandalizi yake yanaanza hivi karibuni. Haitapendeza kuwaacha wafanyakazi kwenye kumbukumbu hii isiyo nzuri (trauma) iendelee kubaki vichwani mwao. Hili linawezekana, tutimize wajibu wetu ili mwaka ujao uwe wa neema

3. Sintofahamu ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Kabla kumbukumbu ya mishahara isiyoridhisha haijapoa, liliibuka jambo lingine linalohusu sintofahamu ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Sintofahamu hii imetokana na mambo makuu yafuatayo;

a. Kubadilishwa utaratibu wa wagonjwa wanaotumia Bima ya Afya kwenye sharti la uhuru wa kwenda kupima afya au kuwaona madaktari ndani ya mwezi mmoja. Bahati nzuri Waziri wa Afya alisitisha utekelezaji wa utaratibu huo lakini haijulikani kitakachofuata baada ya hapo
b. Tishio la kufilisika kwa NHIF kutokana na kile kinachoelezwa kuwa ni kuzidiwa na mzigo wa gharama za magonjwa yasiyoambukiza pamoja na mambo mengine
c. Lawama kwa wachangiaji wa NHIF kwamba wanatumia vibaya dhana ya bima ya afya kwa kuwaweka wanufaika wasiohusika kwenye orodha inayotakiwa hasa wenye umri mkubwa ambao wanahitaji matibabu zaidi

Katika mchakato wa kuboresha mfuko huu wa NHIF, Mh. Rais siku ya Jumapili tarehe 11/09/2022 alitoa matumaini kwa Watanzania kwamba Bunge litapitisha sheria ya Bima ya Afya kwa wote mwezi huu. Kauli hii imepokelewa kwa hisia tofauti; wengine wakiunga mkono moja kwa moja huku wengine wakiunga mkono kwa tahadhari na wengine wakibakia na wasiwasi. Kwa kuzingatia uzoefu wa utendaji kazi wa NHIF, tatizo kubwa ambalo limekuwa likisemwa ni huduma isiyoridhisha. Wengine wanaenda mbali kwa kutamani uwepo wa mifuko huria ili kuondoa ukiritimba wa NHIF. Ipo hofu kubwa pia kwamba kwenye hii Bima ya Afya kwa wote inayotarajiwa, mfanyakazi ndiye atakaebebeshwa zigo lote. Kabla ya Bunge kupitisha sheria hii ya Bima ya Afya kwa wote, ni vizuri likajiridhisha kwamba itakidhi matarajio ya wengi kwa kiasi kikubwa.

4. **Tozo Mpya za Miamala ya elektroniki (Simu na Benki)**
   Mwaka jana, serikali kupitia Bunge ilitunga kanuni za kukusanya tozo kutoka kwenye miamala ya simu za mkononi. Utaratibu huu baada ya kulalamikiwa sana serikali ilipunguza viwango na hivyo kuendelea kutozwa. Mwaka huu tena kanuni zilitungwa ili kupanua wigo wa kukusanya tozo kutoka miamala yote ya kieletroniki ikiwemo Benki. Wadau wengi wameonesha madhara ya tozo katika ustawi wa uchumi na jamii ikiwemo;
   a. Kukata kodi mara mbili kwa wafanyakazi yaani PAYE na tozo yenyewe
   b. Kukata kodi kwenye kipato ambacho hakijazalisha faida
   c. Watu wengi kupunguza utaratibu wa kuweka fedha benki ili kukwepa tozo
   d. Kukusanya malimbikizo ya tozo kwa kukata mishahara na pesa za watu bila taarifa

Kwa vyovyote vile, suala hili la tozo lina athari hasi kwenye ustawi wa uchumi wa Taifa letu na pia kijamii. Zipo ripoti mbili za kuthibitisha hili; ripoti ya Twaweza iliyotolewa Agosti 25, 2022 imeonesha kuwa karibu mara tatu ya watumiaji wa simu wameacha kutuma pesa kwa njia ya simu na pia kiasi cha pesa wanachopokea kimepungua sana. Pia Kampuni ya Simu ya Vodacom ilitoa taarifa yake inayoonesha kwamba wateja Zaidi ya milioni 1.3 wameacha kutumia kabisa huduma ya M-Pesa na mapato kuathirika kwa takribani TZS bilioni 103.8. Taarifa hizi zinaeleza wazi hali halisi na kwamba serikali haihitaji VIASHIRIA vingine juu madhara ya TOZO kwenye uchumi wa Taifa ambayo mwisho wa siku inaharibu pia mahusiano kati ya serikali na jamii. Hivyo basi, tunaungana na wadau wote waliopendekeza tozo hizi kuondolewa na kutafuta vyanzo vingine vya mapato.

5. **HITIMISHO:**
   Ni wakati muafaka serikali kuangalia upya tija na ufanisi wa mbinu zinazotumika kukusanya mapato. Ernest Hemingway anatukumbusha kwamba **"If something is wrong, fix it now".** Tafsiri isiyo rasmi ni kwamba kama jambo haliko sawa litatue sasa. Zaidi sana, ni wakati muafaka Bunge letu kutimiza wajibu wake kwa kuangalia maslahi ya wananchi wanaowawakilisha. Mwisho kabisa, utatuzi wa mambo mengi utafanikiwa kupitia uongozi shirikishi kama Michael Jordan anavyotukumbusha **"Talent wins games, but teamwork and intelligence win championships".**

Nia na Mwelekeo ni kujenga Daima, Taifa kwanza

Paul Loisulie,
Mwenyekiti wa THTU Taifa